


# RAUDHWA MODERN ISLAMIC SCHOOLS

PRE | PRIMARY | SECONDARY | ADVANCE | MADRASSA

## PROSPECTUS

2026



# Karibu Sana

# Raudhwa Modern Islamic Schools



## Neno la Mkurugenzi

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.
Ninayo furaha kuwatambulisha kwenu Raudhwa Modern Islamic Schools, taasisi ya elimu inayolenga kuwajenga vijana katika misingi ya dini, elimu ya kisasa na ujuzi wa maisha.
Katika dunia ya leo, elimu pekee haitoshi bila maadili na stadi za kujitegemea. Ndiyo maana Raudhwa Modern Islamic Schools imeanzishwa kwa lengo la kuwalea wanafunzi wenye maarifa sahihi, tabia njema na uwezo wa kujitegemea.
Tunatoa elimu kuanzia chekechea hadi ngazi ya juu, pamoja na mafunzo ya ufundi na stadi za kazi ili kuhakikisha kila mwanafunzi anapata fursa ya kufanikiwa maishani.
Tunawaalika wazazi, walezi na wadau wa elimu kushirikiana nasi katika safari ya kuijenga jamii bora kupitia elimu na malezi mema.
**Karibuni sana**

Elimu Bora, Malezi ya Kiislamu na Ujuzi wa Maisha

Karibu

# Raudhwa Modern Islamic Schools

## Vision

Kuwa taasisi bora ya elimu ya Kiislamu inayotoa elimu ya kisasa na mafunzo ya stadi za maisha, kwa lengo la kuandaa vijana wenye imani, maarifa, maadili mema na uwezo wa kuji tegemea, kuanzia ngazi ya chekechea hadi chuo kikuu.

## Mission

Kutoa elimu bora inayojumuisha malezi ya Kiislamu, taaluma za kisasa na mafunzo ya ufundi, kwa kuwalea wanafunzi kuwa watu wenye taqwa, nidhamu, ubunifu na ujuzi wa kujitegemea katika jamii.

**Raudhwa Modern Islamic Schools** ni taasisi ya elimu inayotoa malezi ya Kiislamu pamoja na elimu ya kisasa. Lengo la shule ni kuandaa vijana kuwa na maarifa ya dini, elimu ya kitaaluma na ujuzi wa kazi ili waweze kujitegemea na kulitumikia taifa na Umma wa Kiislamu.

**Shule** inalenga kutoa elimu kuanzia ngazi ya chekechea hadi chuo kikuu, pamoja na mafunzo ya ufundi na stadi za maisha.



Karibu

**Raudhwa Modern Islamic Schools**

# Ngazi za Elimu Zinazotolewa

Raudhwa Modern Islamic Schools inatoa elimu katika ngazi zifuatazo:

## Chekechea (Nursery)

Tunatoa Elimu ya Chekechea kwa watoto wenye umri kuanzia miezi tisa hadi miaka mitano. Ngazi hii ina jumla ya ngazi tatu ndogo; Chini, kati na ngazi ya juu (Upper Class)

## Shule ya Msingi

Tunatoa Elimu ya Msingi kuanzia Darasa la Kwanza hadi Darasa la Sita ambapo mitihani ya Upimaji katika ngazi za kimasomo hufanyika ili kupima uelewa wa mwanafunzi.

## Shule ya Sekondari

Tunatoa Elimu ya Sekondari kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Sita ambapo mitihani ya Upimaji katika ngazi za kimasomo hufanyika ili kupima uelewa wa mwanafunzi.

## Mafunzo ya Dini

Wanafunzi watapata mafunzo ya Quran, Tajweed, Hifdh, Kuhifadhi Quran, Fiqh, Aqeedah, Hadith na Maadili ya Kiislamu ili kuwajenga wanafunzi wenye akhlaaq njema na kumcha Mwenyezi Mungu.






## Mafunzo ya Ufundi na Stadi za Maisha

Fauka na elimu ya kawaida, shule pia inatoa mafunzo ya vitendo ili kuwasaidia vijana kujitegemea.

**Kozi zinazotolewa ni:**

- Ufundi Magari
- Umeme
- Plumbing
- Udereva
- Ushonaji
- Kilimo
- Ufugaji
- Mapishi (Catering)


Mafunzo haya yatawasaidia wanafunzi kuwa na ujuzi wa ajira au kujiajiri.

## Maadili na Malezi

Kulingana na mabadiliko ya tabia nchi sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia, shule yetu inasisitiza sana:

- Nidhamu
- Heshima
- Uadilifu
- Uwajibikaji
- Misingi ya dini ya Kiislamu

Wanafunzi watafundishwa kuwa viongozi bora wa jamii.



## Mazingira Bora ya Kujifunzia

Raudhwa Modern Islamic Schools inalenga kuwa na mazingira bora ya kujifunzia ikiwa ni pamoja na:

- Madarasa ya kisasa
- Maabara
- Karakana za ufundi
- Eneo la kilimo na mifugo
- Maktaba
- Msikiti kwa ajili ya ibada



# Muundo wa Uongozi wa Shule

| Nafasi | Majukumu Makuu |
|---|---|
| Mkurugenzi wa Taasisi<br>Director | Atakuwa msimamizi mkuu wa sera, maendeleo na mwelekeo wa taasisi |
| Mkuu wa Shule<br>Head of School | Atasimamia shughuli zote za elimu na uendeshaji wa shule. |
| Makamu Mkuu wa Shule<br>Deputy Head Teacher | Atamsaidia Mkuu wa Shule katika usima mizi wa taaluma na nidhamu. |
| Mkuu wa Taaluma<br>Academic Master/Mistress | Atasimamia ubora wa ufundishaji na matokeo ya wanafunzi. |
| Mkuu wa Nidhamu<br>Discipline Master/Mistress | Atasimamia nidhamu na maadili ya wanafunzi. |
| Mkuu wa Mafunzo ya Dini<br>Islamic Studies Coordinator | Atasimamia masomo ya dini na malezi ya Kiislamu. |
| Walimu wa Masomo Mbalimbali | Watasimamia mafunzo ya stadi za kazi. |
| Mkuu wa Mafunzo ya Dini<br>Islamic Studies Coordinator | Watafundisha masomo ya kitaaluma kwa mujibu wa mitaala. |

## Ngazi ya Juu

| Nafasi | Majukumu Makuu |
|---|---|
| Mkurugenzi wa Taasisi<br>Director | Kiongozi mkuu wa taasisi anayesimamia dira, sera, mipango na maendeleo ya shule. |
| Afisa Tawala<br>Administrative Officer | Atasimamia masuala yote ya utawala, rasilimali watu, nyaraka na mawasiliano ya taasisi |
| Meneja wa Shule<br>School Manager | Atahusika na uendeshaji wa kila siku wa shughuli za shule, ikiwemo fedha, miundo mbinu na huduma. |
| Mthibiti Ubora Mkuu<br>Chief Quality Assurance Officer | Atasimamia ubora wa elimu, mitaala, ufundishaji na kuhakikisha viwango vya shule vinazingatiwa. |
| Mthibiti Ubora Mkuu<br>Chief Quality Assurance Officer | Atasimamia ubora wa elimu, mitaala, ufundishaji na kuhakikisha viwango vya shule vinazingatiwa. |

## Ngazi ya Uendeshaji wa Shule

| Nafasi | Majukumu Makuu |
|---|---|
| Makamu Mkuu wa Shule<br>Deputy Head Teacher | Atamsaidia Mkuu wa Shule katika usimamizi wa taaluma na nidhamu. |
| Mkuu wa Taaluma<br>Academic Master/Mistress | Atasimamia ratiba, ufundishaji na maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi. |
| Mkuu wa Nidhamu<br>Discipline Master/Mistress | Atahakikisha nidhamu, maadili na mwenendo mzuri wa wanafunzi. |
| Mkuu wa Mafunzo ya Dini<br>Islamic Studies Coordinator | Atasimamia masomo ya dini, Qur'an na malezi ya Kiislamu. |
| Mkuu wa Mafunzo ya Ufundi<br>Vocational Training Coordinator | Atasimamia kozi zote za ufundi na stadi za maisha. |

## Ngazi ya Walimu na Wakufunzi

| | |
|---|---|
| Walimu wa Masomo ya Kitaaluma | Watafundisha masomo ya kawaida kwa kufuata mitaala ya elimu. |
| Walimu wa Dini<br>Islamic Teachers | Watafundisha masomo ya Kiislamu na Qur'an. |
| Wakufunzi wa Ufundi<br>Vocational Instructors | Watasimamia mafunzo ya vitendo kama vile Ufundi Magari, Umeme, Plumbing Udereva, Ushonaji, Kilimo na mifugo na Mapishi |

## Ngazi ya Msaada

| Nafasi | Majukumu Makuu |
|---|---|
| Mhasibu<br>Accountant | Atasimamia mapato na matumizi ya fedha za shule. |
| Karani<br>Secretary | Atahusika na utunzaji wa kumbukumbu, nyaraka pamoja na mawasiliano ya ofisi. |
| Walezi<br>Matron/Patron | Watatunza ustawi wa wanafunzi hasa wa bweni. |
| Walinzi<br>Security Guards | Watalinda usalama wa shule na mali zake. |
| Wafanyakazi wa Huduma<br>Support Staff | |

## Hitimisho la Muundo

**Muundo huu umeandaliwa ili kuhakikisha:**

- ☑ Ufanisi katika uongozi
- ☑ Uwajibikaji katika kila ngazi
- ☑ Ubora wa elimu na malezi
- ☑ Uendeshaji wa kitaalamu wa taasisi




# Sheria na Kanuni za Shule

**Ili kuhakikisha mazingira mazuri ya kujifunzia, wanafunzi wanapaswa kufuata kanuni zifuatazo:**


1. Kuheshimu walimu, wafanyakazi na wanafunzi wenzao.
2. Kudumisha nidhamu na tabia njema wakati wote.
3. Kufika shuleni kwa wakati na kuhudhuria vipindi vyote.
4. Kuvaa sare rasmi ya shule kwa usafi na nidhamu.
5. Kutunza mali za shule.
6. Kuepuka vitendo vya fujo, matusi au tabia zisizofaa.
7. Kuhudhuria ibada na shughuli za dini kama ilivyopangwa.
8. Kufanya bidii katika masomo na shughuli za shule.




## Fursa na Shughuli za Wanafunzi

Katika shule za Raudhwa Modern Islamic, wanafunzi watapata fursa ya kushiriki katika:


- ☑ Mashindano ya kitaaluma
- ☑ Mashindano ya Quran
- ☑ Michezo mbalimbali
- ☑ Kilimo na ufugaji wa vitendo
- ☑ Mafunzo ya uongozi
- ☑ Mafunzo ya ufundi na stadi za maisha



## Wito kwa Wazazi na Walezi

**Raudhwa Modern Islamic Schools** inaamini kuwa ushirikiano kati ya shule na wazazi ni muhimu katika malezi ya mwanafunzi.

**Tunawahimiza wazazi** Kufuatilia maendeleo ya watoto wao pamoja na Kushirikiana na walimu katika malezi




## Hitimisho

Raudhwa Modern Islamic Schools inalenga kuwa kitovu cha elimu bora, maadili mema na stadi za kujitegemea kwa kizazi kipya.

Kupitia elimu hii, tunaamini kuwa wanafunzi wetu watakuwa viongozi bora, wabunifu na watu wenye manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla wake.

Raudhwa Modern Islamic